

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



WIZARA YA
ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA

TAASISI YA TEKNOLOJIA
DAR ES SALAAM



MAHAFALI YA KUMI NA TANO YA TAASISI

Mkuu wa Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam (DIT) anawatangazia wahitimu na wadau wote wa DIT kuwa Mahafali ya Kumi na Tano (15) ya Taasisi yamepangwa kufanyika Alhamisi, tarehe **2 Desemba, 2021**.

Mahafali hayo yatatanguliwa na siku ya utoaji tuzo kwa wanafunzi waliofanya vizuri katika masomo yao katika mwaka wa masomo 2020/2021, sherehe ambazo zitafanyika Jumatano, tarehe **1 Desemba, 2021**.

Taasisi inapenda kuwataarifua wahitimu wa Shahada ya Uzamili (M.Eng), Shahada ya Kwanza (B.Eng/B.Tech) na Stashahada ya Uhandisi na Teknolojia (OD) kusoma utaratibu na hatimaye kuthibitisha ushiriki wao katika Mahafali hayo kupitia akaunti zao za **SOMA** (soma.dit.ac.tz).

Wahitimu watakaoshiriki wanapaswa kulipia joho la Mahafali Tshs. 50,000/= (kwa wahitimu wa Shahada ya Uzamili) na Tshs. 30,000/= (kwa Wahitimu wa Stashahada za Uhandisi na Teknolojia (OD) na wale wa Shahada za Kwanza za Uhandisi na Teknolojia Bachelor).

Wahitimu watakaoshiriki ambao majina yao yapo kwenye tovuti ya Taasisi (www.dit.ac.tz) watajaza fomu maalumu ya kuthibitisha ushiriki wao na kupatiwa control number kwa ajili ya malipo kupitia simu zao za mkononi na katika mtandao wa **SOMA** na kisha walipe. *Watakaoruhusiwa kushiriki Mahafali haya ni wale tu watakaokamilisha usajili wao.*

Kila muhitimu ahakiki uwepo wa jina lake kwenye orodha iliyotolewa hata kama hatahudhuria kwenye sherehe za mahafali kwani transcripts na vyeti vitatolewa kwa walioorodheshwa tu.

ZINGATIA: Malipo yafanyike kwa kutumia jina kamili kama linavyoonekana kwenye orodha ya wahitimu wa mwaka 2020/2021 iliyopo kwenye tovuti ya Taasisi, namba ya usajili na madhumuni ya malipo yaani Mahafali.

“Rehersal” itafanyika Jumatano, tarehe **1 Desemba, 2021 - Saa 8** Kamili Mchana.

Mwisho wa kuthibitisha ushiriki na kulipia ni tarehe **25 Novemba, 2021**. Hakutakuwa na muda wa nyongeza baada ya tarehe hii.

Atakayeona tangazo hili anaombwa kumjulisha mwenzake.

Tangazo hili limetolewa na:

**Ofisi ya Uhusiano,
Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam,
S.L.P 2958,
Dar es Salaam.**